# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 7 Juni, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

*(Hapa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni waliondoka Ukumbini)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Ritta Kabati, kwa niaba yake.

Na. 313

### Kukamilika kwa Mradi wa Usambazaji Maji Wilaya ya Iringa Vijijini

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA)** aliuliza:-

Katika miaka ya 1990, Wilaya ya Iringa Vijijini kulikuwa na mradi wa usambazaji wa maji kwa kutumia chanzo cha maji ya Mto Mtitu ili kuondokana na adha ya maji inayowakumba wananchi wa Iringa Vijijini; juhudi za kufanya upembuzi yakinifu zilifanyika ili kuweza kusambaza maji kwa *gravity* kwenye vijiji vyote vya Kata za Maguliwa, Luhota, Mseke, Ifunda, Mgama na Maboga:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi huu ili kuweza kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wa Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, imepanga kufanya usanifu wa kina wa mradi mkubwa wa maji ambao utahusisha vijiji vya Kata za Ngawila, Luhota, Mseke, Ifunda, Mgama na Lugonga. Lengo ni kubaini uwezo wa chanzo cha Mto Mtitu katika kuhudumia maeneo hayo yote. Kazi hiyo imepangwa kufanyika katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, ambapo zimetengwa Shilingi milioni 49.5. Mradi huo utakapokamilika, jumla ya vijiji 17 vyenye wakazi wapatao 36,397 vitanufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba niulize maswali mawili tu ya nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Iringa hasa katika Wilaya za Kilolo, Iringa Vijijini, Isimani, Kalenga na Mufindi, miradi mingi sana ya maji imekuwa haikamiliki kwa wakati na kusababisha wanawake wengi sana hata ndoa zao zimekuwa hatiani kwa sababu ya baridi; wamekuwa wakiamka asubuhi sana kwenda kutafuta maji. Je, ni lini sasa miradi ile iliyopo katika Mkoa wetu wa Iringa, Serikali itafanya kwa uharaka zaidi, pamoja na kuponya ndoa za wanawake wa Iringa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wakandarasi wengi sana wamekuwa wakikamilisha miradi, lakini Serikali imekuwa haiwalipi madai yao kwa wakati. Je, ni mkakati gani umewekwa na Serikali kuhakikisha Wakandarasi hawa wanalipwa kwa wakati ili hii miradi iweze kukamilika kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa pole sana kwa wale ambao ndoa zao zimeingia hatiani, mashakani kwa hiyo changamoto ya maji. Naomba niwasihi akinababa kwamba hawa akinamama msiwahukumu katika hilo kwa sababu wanachokifanya ni kuwatafutia maji watoto na ninyi akinababa wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza ni kwamba lini miradi hii itakamilika? Katika vipindi mbalimbali nimeelezea hapa, ni kweli miradi mingi ya

maji imechelewa kukamilika kwa muda na watu mnafahamu ile miradi ya *World Bank* hasa tuliyokuwa tukiitekeleza katika kipindi kilichopita ambayo mpaka sasa tunaendelea nayo, ni kwamba miradi mingi Wakandarasi waliweza kutoa vifaa kutoka *site,* ni kwa sababu Wakandarasi wengi sana wali-*raise certificate* lakini walikuwa hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kama nilivyosema awali, ni kwamba, kwa sababu mwaka uliopita ulikuwa ni wenye changamoto kubwa sana, kwani fedha za miradi hazikwenda vizuri. Kama nilivyosema, katika Serikali hii ya Awamu ya Tano jukumu lake kubwa lilikuwa ni kukusanya kodi na mnafahamu kwamba tokea mwezi wa 12 mpaka hivi sasa, makusanyo ya kodi kila mwezi tumevunja rekodi ukilinganisha na kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana *certificate* zote zilizokwenda katika Wizara ya Maji, zimelipwa na hata Naibu Waziri wa Maji juzi juzi hapa alikuwa anasema kwamba Mkandarasi yeyote mwenye *certificate* ambaye anatakiwa alipwe, afikishe haraka Wizara ya Maji pesa hizo zitalipwa. Ndiyo maana wale Wakandarasi wote waliokuwa hawajalipwa mwanzo, sasa hivi wote wamelipwa. Imani yetu kubwa ni kwamba sasa miradi hiyo itakwisha kwa sababu Wakandarasi wote wako *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madai yao kwamba ni lini yatalipwa? Ndicho nilichokisema hapa katika majibu yangu ya awali, kwamba sasa pesa zote za Wakandarasi wote zimeshapelekwa katika Halmashauri. Tunachohitaji ni kwamba zile *certificate* ambazo Wakandarasi wamelipa, Wakurugenzi wa Halmashauri wafanye haraka waweze kulipwa pesa zao ilimradi kwamba ile miradi iweze kukamilika na wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Swali; je, wale Wakandarasi au Halmashauri zilizolipa pesa kwa Wakandarasi hewa, mtachukua hatua gani? Kuna miradi kadhaa katika Wilaya ya Nkasi ambayo pesa zililipwa lakini hakuna kilichofanyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mkandarasi amelipwa lakini kazi hajafanya, maana yake huo ni wizi; jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie na hili tumelisema katika vipindi mbalimbali, Wakandarasi wowote ambao kwa njia moja au nyingine

wamechukua fedha na kazi wametelekeza, tutahakikisha, nami nitawaomba Wakurugenzi wote waweze kuwabainisha; hasa wale Wakandarasi wa maji waliotekeleza miradi katika maeneo yao. Kwa sababu tukirejea katika Bunge lililopita, Waziri wa Maji hapa alisema wazi kwamba Wakandarasi ambao watashindwa kutekeleza wajibu wao watafutiwa hata suala la kupata tenda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy, naomba tukitoka hapa unipe rejea ya hao Wakandarasi ili mradi tuweze kuwafanyia kazi. Lengo kubwa ni kwamba, wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, hoja ya Mheshimiwa Keissy ndiyo tumeshaanza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji tumeamua kuchukua hatua kwamba hatuwezi kupeleka hela kwenye Halmashauri mpaka walete *certificate*. Tumefikia hili kwa sababu hela zilikuwa zinapelekwa, halafu zinatumika, lakini ukienda kule hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza huko nyuma katika Bunge hili, ni kwamba tunakwenda kuunda Kamati ya Wataalam. Utaleta *certificate* yako kabla hatujailipa, tutatuma wataalam kwenye eneo twende tukaangalie kama hiyo kazi imefanyika ili tuweze kupambana na hili suala ambalo lilitaka kutupeleka pabaya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kufahamu, kule Jimboni Mbulu kuna Bwawa la Dongobesh lililokamilika takriban miezi sita. Mkandarasi ameshaleta *certificate* yapata miezi miwili. Waheshimiwa Mawaziri wanajibu majibu hapa, lakini kule Wizarani hakuna mchakato wa kuwalipa hao Wakandarasi. Naomba, kama itawezekana, Waziri ana kauli gani kumlipa Mkandarasi wa Bwawa la Dongobesh? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Dongobesh ni kweli ujenzi wake umeshakamilika, kilichobaki ni miundombinu ili lile bwawa sasa liweze kufanya kazi kwenda kumwagia kwenye mashamba. Tumeweka utaratibu kwamba *certificate* zifike. Wiki iliyopita

niliongea na Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka wiki iliyopita *certificate* zilikuwa hazijawasilishwa katika Wizara, lakini tunaendelea kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshamwagiza Mkurugenzi wa Maji Vijijini ili aweze kuwasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbulu Vijijini ili waweze kuangalia hizi *certificate* ziko wapi, kwa sababu kule wanasema zimetumwa, lakini Wizarani hazijafika. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala tunalifanyia kazi na pindi *certificate* zikifika hela tunazo, tunalipa, ili hili bwawa liweze kukamilishwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 314

**Kuupitia Upya Mfumo wa Ugatuaji wa Madaraka**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Kuwepo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya nchini kumekuwa kukileta migongano katika utekelezaji wa sera na shughuli mbalimbali za maendeleo nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuupitia upya mfumo wa ugatuaji wa madaraka *(D by D)* ili kuweza kuuboresha na kupunguza migongano mbalimbali ya kiutendaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa wapo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Ibara ya 61(1) mpaka (5) na majukumu yake yamefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 61(4) kwamba atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma *(Decentralization by Devolution)* pia inatokana na Ibara ya 145 na 146. Madhumuni yake ni kupeleka madaraka kwa wananchi yakiwemo madaraka ya kisiasa, kifedha, kiutawala ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Mkuu

wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni wasimamizi wa sera, sheria, kanuni na miongozo katika Mikoa na Wilaya wanayoongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi hao kisheria hawaruhusiwi kuingilia *(interference)* maamuzi na utendaji wa Serikali za Mitaa endapo hakuna sheria au taratibu zilizokiukwa kimaamuzi. Hata hivyo, wamepewa mamlaka na sheria kuingilia kati *(interventions)* endapo maamuzi yatakayofanywa na Serikali za Mitaa yatakiuka sera, sheria na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa yamebadilika kutoka kwenye dhana ya utoaji amri na upokeaji amri au mdhibiti na mdhibitiwa, kuwa ya mashauriano, majadiliano na maelewano. Vilevile, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kufanya vikao vya pamoja na Wizara za Kisekta ili kuwa na uelewa wa pamoja wa dhana ya ugatuaji na mantiki yake katika kusogeza karibu huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mfumo wa ugatuaji wa madaraka ulikuwa na lengo la kuwapa madaraka wananchi kuweza kuwa na maamuzi yao na kutekeleza masuala yao yanayohusiana kufuatana na mazingira yaliyopo; na kwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamekuwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu hayo katika maeneo husika: Je, Serikali haioni haja ya kuupitia upya huu mfumo ili Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndio wabaki badala ya kuwa na Wenyeviti wa Halmashauri za Miji, Halmashauri za Wilaya pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri za Majiji ambao kidogo wamekuwa wakiongeza gharama kwenye Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kwa kuwa Ofisi za Wakuu wa Wilaya sasa hivi zimekuwa zikikabiliwa na upungufu mkubwa sana wa mapato na kwa sababu Serikali kuu imekuwa haina fedha za kutosha kuweza kuzipatia hizo Wilaya. Je, Serikali haioni haja kwamba Wakuu wa Wilaya sasa iwe ni sehemu ya kutegemea mapato yanayotokana na hizo Halmashauri ili waweze kuendesha majukumu yao na kusimamia sera vizuri katika maeneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeelezea pale awali maeneo haya mawili; nafasi

za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 61 na ile ya Serikali za Mitaa Ibara ya 145 na 146.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ikiwezekana basi hizi nafasi nyingine zitolewe. Kutokana na Katiba hiyo sasa zimekwenda kutungwa sheria. Kuna Sura namba 287 na 288, ambapo 287 inaelekeza katika Halmashauri, kuonyesha *structure,* jinsi gani kama Mwenyekiti wa Halmashauri, Diwani na kiongozi wa ngazi ya Kijiji anayechaguliwa ndiyo maana ya ile dhana kubwa ya *D by D* kushusha madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema uondoe hilo, maana yake umetoa dhana ya *D by D.* Kwa hiyo, maana yake ni Katiba sasa imetupeleka katika utengenezaji wa sheria ambapo leo hii kijiji kinahakikisha kina Mwenyekiti wake wa Kijiji na Mwenyekiti wake wa Vitongoji, wanafanya maamuzi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, jukumu lao kubwa ni kusimamia utaratibu na kanuni kuhakikisha kwamba unaendelea kama ilivyo. Kwa hiyo, kitendo cha kuondoa kimojawapo, maana yake, kwanza utakuwa umevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini Sheria za Bunge ambazo zimewekwa humu kwa mujibu wa sheria itakuwa inaonekana hatuko sawasawa. Naamini kwamba mfumo tuliokuwa nao hivi sasa uko sawasawa. Kama kutakuwa na mawazo mengine, basi tutaendelea kuboresha kwa kadri siku zinavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la Wakuu wa Wilaya kwamba hawana mapato na mapato yao ikiwezekana yanayotoka kwenye Halmashauri ndiyo yangeweza kuwasaidia kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa ni kwamba, tunajua Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wakati mwingine wanakuwa na changamoto kubwa sana kwenye *OC*. Jukumu letu kubwa sisi kama Ofisi ya Rais ni kuhakikisha tunaziwezesha ofisi hizi. Kitendo cha mfano, hata hatukipendi sana, saa nyingine kitendo cha Mkuu wa Wilaya kwenda kuomba kwa Mkurugenzi kupewa pesa ya mafuta, mwisho wa siku anashindwa hata kuisimamia Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jukumu la Serikali Kuu na sisi tutajitahidi, ndiyo maana tunasema kwamba tufanye *collection* ya mapato. Serikali Kuu inavyopata fedha za kutosha zitasaidia ku-*facilitate* kazi zake kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa ziweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, nataka niongezee majibu hayo katika swali lililoulizwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema yeye angependekeza kwamba hawa Wenyeviti wa Halmashauri waondoke na badala yake, kazi zile kwa sababu zinafanywa kwa pamoja katika dhana ya ugatuaji wa madaraka kwenye Halmashauri, basi Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawa wachukue nafasi ile. Nataka tu niseme kwamba kusema ukweli hapa itakuwa imekiuka dhana ya *checks and balances* kwa sababu Wenyeviti ni Wawakilishi wa wananchi na wao ndiyo *political figures* kwenye maeneo yale, kwa maana ya uwakilishi wa wananchi *per se*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Wawakilishi wa Serikali Kuu. Kazi yao, pamoja na kazi nyingine ni kuziangalia hizi Halmashauri kama zinafuata sera, sheria za nchi, kanuni, taratibu na maagizo mbalimbali ya Serikali Kuu, pale chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanamwangalia nani? Wanamwangalia huyu Mwakilishi wa wananchi ambaye yuko pale na wataalam wake hawa kuanzia Mkurugenzi na wataalam wengine kama wanafanya vizuri. Ndiyo maana tunasema, hakuna mwingiliano kwa sababu mwingiliano ni pale ambapo Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anaingilia jambo ambalo linakwenda vizuri. Huo ni mwingiliano; lakini anapofanya *intervention* ya jambo linalokwenda vibaya ili sheria izingatiwe, hii inaruhusiwa kwa sababu ndiyo kazi yake iliyomweka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niongezee majibu haya na niwahakikishie kwamba mfumo wetu sisi Watanzania wa ugatuaji wa madaraka ni mfumo mzuri ambao nchi nyingi za Kiafrika zinakuja kujifunza hapa kwa sababu ni mfumo uliokaa vizuri na unasababisha amani na utulivu katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuendelee nao huu hadi hapo baadaye ingawa tunakubali kwamba huwa kuna *reforms* zimekuwa zikifanyika kuanzia mwaka 1982, mwaka 1992, mwaka 1998, lakini ipo haja ya kuendelea kuboresha lakini siyo katika eneo hili la *checks and balances.* Tutaharibu *system* nzima ilivyokaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Nkamia, ahsante. Najua umenikosea kwa sababu leo niko tofauti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza. Wala sina tatizo lolote na Wakuu wa Wilaya, lakini kama Serikali Kuu inashindwa kumhudumia Mkuu wa Wilaya, anakwenda kuomba Halmashauri ambayo inaongozwa na Mkurugenzi, hiyo *checks and balances* inatoka wapi? Haoni kwamba Wakuu wengi wa Wilaya watakuwa ni ombaomba sasa kwa sababu *OC* wanazopata ni kidogo na matokeo yake wanaishi kwa kutegemea fadhila za Wakurugenzi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI,

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa kuna maelezo kwa baadhi ya maeneo kwamba Wakuu wa Wilaya wanawaomba mafuta Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi *formally* yaani kupata taarifa rasmi kwa maana ya kwamba hilo linatokea na kwamba limekubalika, kweli jambo hilo halipo. Kwa hiyo, kama linatokea pengine ni kwa kesi fulani fulani tu, lakini kusema ukweli kwanza hatulikubali na haliruhusiwi kwa mujibu wa sheria. Pia kama linafanyika, linakiuka sheria. Kwa hiyo, niseme tu, siwezi kuridhia udhaifu huu mpaka tufanye utafiti tujue kweli hili jambo linatokea? Kama linatokea, nini tufanye kwa kuzingatia hili linalosemwa na Mheshimiwa Mbunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani jambo hili siyo maeneo yote tuka-*generalise* kwamba sehemu zote inatokea, siyo kweli. Pia kama linatokea, linakiuka taratibu, kanuni na sheria za mgawanyo wa madaraka na majukumu na *the principle of checks and balances. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, labda mliangalie na maeneo mengine, kwa sababu limesikika katika maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Oliver Semuguruka. *(Makofi)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa zana ya *D by D* inaonekana bado haieleweki hata kwa sisi Wabunge; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ikiwemo sisi Wabunge na Madiwani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hii dhana imekuwa ni dhana ngeni, japo imeanza muda mrefu; lakini hata ukifanya rejea, wakati mijadala yetu katika bajeti mbalimbali za sekta unaona kwamba hata Waheshimiwa Wabunge, ile

*concept* nzima ya *D by D* bado haijakaa vizuri. Leo hii tulivyokuwa tukijadili katika Wizara ya Elimu, tulivyokuwa tukijadili katika Wizara ya Afya, ukiangalia michango ya Wajumbe wengi sana dhana ya *D by D* haijakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana hata katika kikao chetu tulivyokuwa tukifanya na Wizara ya Afya, Wataalam na sisi Viongozi Wakuu tulivyokuwa tukibadilishana mawazo tukasema ni vyema sasa dhana hii kwanza ikiwezekana iingie hata kwa watu walioajiriwa wa Serikali, wajue falsafa halisi ya dhana ya *D by D*. Maana yake katika Mpango huu imetupa changamoto pana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutaangalia jinsi gani tutafanya ili mradi hata Wabunge na Waheshimiwa Madiwani wote kwa pamoja na Watumishi wote wa Serikali wajue nini *concept* ya *D by D*? Nini maana ya dhana ya kurudisha madaraka kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja yake ni ya msingi, nadhani tutaifanyia kazi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba uelewa siyo mzuri sana kwenye dhana hii ya ugatuaji wa madaraka, nami napendekeza tu kwa sababu dhana hii ina maudhui makubwa sana katika msingi wa utawala wa nchi yetu. Inapokuwa haieleweki, inasababisha hata mijadala wakati mwingine kutoka nje ya *context* na pengine siyo kawaida kuonekana pengine mjadala huo anayetoa kwenye *context* ni mtu ambaye ana nafasi kubwa na kwamba jambo hili lipo kikatiba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napendekeza na pengine naomba kwa kupitia swali hili tuone utaratibu kwa sisi Serikali na Bunge; namna ya kufanya kwanza semina hata kwa Wabunge wote kabisa kwenye jambo hili. Mfanye semina na ikibidi kile Chuo chetu cha Uongozi ndiyo kije kituwezeshe katika jambo hili na kama tuna Wataalam ndani ya Serikali tunaweza tukatoa Watalaam, lakini kama kuna wataalam ndani ya Bunge, tutoe. Kwa sababu jambo hili kwa mimi ambaye ni mwanataaluma wa eneo hilo, napata nalo shida sana. Kusema ukweli *context* imepotea kabisa kwa sababu watu wanatafuta hata kwa upungufu fulani wanafikiri *solution* ni ku-*centralize* tena badala ya ku-*decentralize*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tuone namna bora ya kuweza kufanya semina kubwa nzuri ya watu kupata uelewa juu ya jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nadhani hilo la upande wa Serikali, ninyi mtatutaarifu mkishakuwa tayari, halafu sisi tutachukua hatua. Mheshimiwa Mary Chatanda. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Wakuu wa Wilaya ndiyo Watendaji Wakuu ambao wanakutana na wananchi kwa karibu zaidi. Je, Waziri anaweza sasa kufanya mabadiliko badala ya kupeleka *OC* kwa *RAS* wakapeleka moja kwa moja kwa *DAS* ili kusudi waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba jambo hili tumeliona na pengine liko dhahiri sana. Kwa sababu kule kuna Mkuu wa Utawala katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Pia kuna Mkuu wa Utawala katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye *RAS* na huku anaitwa *DAS* ambao kazi yao na majukumu tofauti ni maeneo tu. Kwa hiyo, sidhani kama kuna ubaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema wakati wa majumuisho yangu siku ya bajeti yangu kwamba tunaangalia namna ya kuhakikisha kwamba *OC* hizi kwenye Wilaya zinapelekwa moja kwa moja, nasi tumekubaliana. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017, *OC* hizi kwenye Wilaya zitapelekwa moja kwa moja kwenye Ofisi za Ma-*DAS* ili na wenyewe waweze ku-*manage* pale kama wanavyoafanya Mkoani. Kusema ukweli tunalichukua wazo hili, ni zuri nasi tulishawekea mkakati wake, tutalitekeleza, ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Martin Alexander Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 315

**Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami kwa Ufadhili wa umoja wa Ulaya-Mbinga**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Wilaya ya Mbinga imebahatika kupata mradi wa kujenga barabara ya lami toka Kijiji cha Longa hadi Kijiji cha Litoha kwa kiwango cha lami kwa ufadhili wa Umoja wa Nchi za Ulaya na mradi huo umeshaanza kutekelezwa:-

(a) Je, ujenzi wa mradi huo unategemewa kukamilika lini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi waliotoa mashamba na nyumba zao kupisha ujenzi wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Mtonda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara awamu ya kwanza kutoka Longa hadi Bagamoyo ulianza tarehe 1/10/2015 na unategemewa kukamilika tarehe 30/6/2016. Hata hivyo, kutokana na mvua kubwa zilizonyesha Wilaya ya Mbinga, Mkandarasi alishindwa kufanya kazi kama ilivyokuwa imepangwa hali iliyolazimu kuongeza muda hadi tarehe 30/9/2016. Sehemu ya pili inaanzia Kijiji cha Bagamoyo hadi Kijiji cha Lutoho chini ya Mkandarasi *GS Contractors Limited* ambaye mkataba wake ulianza tarehe 1/5/2016 na unategemewa kumalizika tarehe 30/1/2017.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, sharti lilitolewa na Umoja wa Ulaya ili waweze kujengewa barabara ya lami kutoka Longa hadi Bagamoyo lilikuwa ni kutokuwepo kwa fidia. Halmashauri kwa maana ya Madiwani walifanya uhamasishaji wa kutoa elimu kwa wananchi ili kukubali mradi huo na wote waliridhia ndiyo maana barabara hiyo imeanza kujengwa. Serikali inawapongeza viongozi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla kwa kukubali kuupokea mradi huo kwa ustawi wa uchumi wa maendeleo ambayo ni uzalishaji mkubwa wa kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msuha swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nami pia niungane na Serikali kwanza kuwapongeza wananchi wa Kata za Mkumbi, Kata za Kipololo na Ukata ambao walikubali kupisha mradi huu kwa ustawi wa uchumi wa Wilaya yetu. Hata hivyo nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa upana wa barabara hii, barabara hii inaanzia Mbinga Mjini inapita Litowo lakini pia inaunganisha na Wilaya ya Nyasa. Mfadhili amekubali kujenga kutoka Longa hadi Litoho; kuna kipande cha kilomita 15 kutoka Mbinga Mjini haji Kijiji cha Longa. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutumia nguvu zetu za ndani ili kukamilisha kipande hiki cha kutoka Mbinga Mjini hadi Longa chenye umbali wa kilomita 15?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara yetu inayotoka Mbinga Mjini kwenda Hospitali ya Litembo kupitia Kijiji cha Tanga – Uyangayanga - Kindimba - Mundeki ni muhimu sana kwa vile Hospitali hii inatumika kama Hospitali yetu ya Rufaa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuijenga barabara hii inayoelekea Hospitali ya Rufaa ya Litembo ili kurahisisha huduma za afya katika eneo hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami nawapongeza sana wananchi hawa kwa sababu barabara hii ina *Euro* karibu milioni nne ambayo ukipiga mahesabu inaenda karibu shilingi bilioni kumi na eneo lile nadhani Mheshimiwa Mbunge anafahamu, kwanza kuna changamoto kubwa sana ya milima; lakini tumepata ufadhili mkubwa, kwa hiyo, hata zao la kahawa sasa watu watakuwa na fursa ya kuweza kusafirisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lake ni kwamba hiki kipande cha katikati cha kutoka Mbinga Mjini mpaka Longa ambacho kina kilomita 15 ni jinsi gani tutafanya sasa kipande hiki kiweze kuunganishwa? Mheshimiwa Mbunge, tumelisikia hili, lakini naomba michakato hii sasa ianze katika bajeti kuonyesha kwamba kuna uhitaji kutoka Halmashauri husika, nasi tutaangalia kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba barabara hii, hiki kipande cha kilomita 15 bajeti yake itakuwa ni kubwa, lakini nadhani kwanza muanze kuangalia jinsi ya kufanya kwamba Halmashauri ionyeshe kipaumbele katika eneo hilo. Katika mchakato wa bajeti, Serikali itaangalia namna ya kufanya ili eneo hilo sasa liweze kupewa kipaumbele, angalau kipande cha lami kiweze kuunganishwa na mwisho Nyasa na Mbinga iweze kuunganika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusema kutoka Mbinga Mjini mpaka Kihesa ambako kuna Hospitali, wananchi wanapata huduma pale, vilevile naomba nirejee katika jibu langu la kwanza kwamba tuweke kipaumbele na Serikali haitasita kuona kwamba kwa sababu ni maeneo ambayo wananchi wanapata huduma hasa ya afya, nasema kipaumbele hiki lazima tukifanyie kazi.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi ile anayoendelea kuifanya na Madiwani wake, waweke katika mpango, Serikali itaujadili kwa kina na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI hatutasita kushirikiana na Halmashauri ya Mbinga kuhakikisha maeneo haya yanapata huduma kama maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Suala la fidia ambalo linawakabili wananchi wa Mbinga Vijijini katika kupisha ujenzi wa barabara ya lami, ndilo pia linalowakabili wananchi wa Jimbo la Mwibara ambako kuna barabara ya lami ya Nyamuswa – Bunda - Kisolia - Nansio inajengwa kilomita 50 kutoka Bulamba kwenda Kisolia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alitembelea ujenzi wa barabara ile akaahidi kwamba wananchi wale watalipwa fidia. Sasa nataka kupata majibu ya Serikali, wananchi wa Mwibara wategemee lini wataweza kulipwa fidia zao kwa nyumba zilizobomolewa na mashamba yaliyopitiwa na barabara ya lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikiri, kaka yangu Mheshimiwa Lugola amechomekea hapa vizuri sana. Kwa sababu barabara hizi zina sura tofauti. Hii barabara anayosema Mheshimiwa Kangi Lugola iko chini ya Wizara ya Miundombinu na huku tunazungumzia barabara ya Halmashauri ambayo ilipata ufadhili maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifanya rejea, siku ya Wizara ya Miundombinu, swali hili liliulizwa vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge huko. Nadhani lilitolewa ufafanuzi kwamba Serikali itahangaika kutafuta fedha, pale itakapokuwa mambo yamekamilika, wananchi watalipwa fidia; kwa mujibu wa rejea ninayoifanya ya siku hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina imani kwamba maswali yale au majibu yale yaliyokuwa yanafanyiwa rejea siku ya Wizara ya Miundombinu, yatabaki vilevile. Naomba nikiri wazi, Kangi Lugola kwa sababu ni mpiganaji mzuri sana, kilio chake kitakuwa kimesikika vizuri na Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge pale nyuma sijaweza kujua ni nani, tafadhali taja jina lako.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Alex Raphael Gashaza, ni Mbunge wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa barabara ya Murugarama Lulenge mpaka Mzani kilomita 85 iliahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne mwaka 2012, lakini barabara hiyo imeahidiwa tena na Rais wa Awamu ya Tano wakati wa Kampeni mwaka 2015 na ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lakini katika bajeti

hii ya 2016/2017 haipo kwenye bajeti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge tumeongea naye kwa muda mrefu, tulikutana na Waziri wa Ujenzi na baadaye tukaomba twende tukakutane na Katibu Mkuu. Kwa kweli anafuatilia sana ujenzi wa hii barabara. Namshukuru sana na naomba aendelee na juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tulikuwa tumemwambia na naomba kurudia ni kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais na ahadi za Viongozi wengine wote zilizotolewa na zile ambazo zimewekwa katika Kitabu cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015 hadi 2020, Serikali hii ya Awamu ya Tano itazitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotekea, kwa nini mwaka huu fedha hazikutengwa, ni kwa sababu tu tulitoa kipaumbele kwa zile barabara ambazo zilishaanza kujengwa na Wakandarasi wako *site* na Serikali inapoteza fedha kuwalipa watu ambao hawafanyi kazi. Tulitaka barabara hizi kwanza zikamilike, halafu kuanzia mwaka ujao wa fedha tutaanza kuingia katika maeneo mapya ambayo viongozi wetu wakuu waliahidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nadhani utakuwa umeona sasa hili suala la *D by D* linavyoleta tabu; kwa sababu sasa hatujui ni Waziri yupi anajibu kwenye barabara ipi?

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, sasa aulize swali lake.

Na. 316

**Ahadi ya Barabara za Lami Katika Jimbo la Mtera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Jimbo la Mtera katika Kijiji cha Mvumi-Misheni aliahidi kutujengea barabara ya lami kutoka Mlowa Barabarani hadi Mvumi-Misheni kwenye Hospitali Teule ya Wilaya ya Chamwino. Pia Rais wa Awamu ya Tano katika kampeni zake alipofika Mvumi-Misheni alisisitiza kuwa barabara hiyo itajengwa haraka iwezekanavyo. Je, ujenzi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Jimbo la Mtera katika Kijiji cha Mvumi – Misheni aliahidi kujenga barabara ya lami kutoka Mlowa Barabarani hadi Mvumi- Misheni kwenye Hospitali Teule ya Wilaya ya Chamwino. Aidha, ni kweli kuwa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Rais wa Awamu ya Tano, naye aliahidi kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kwa jamii na hususan katika kusaidia wagonjwa wanaoenda kupata huduma ya matibabu katika Hospitali ya Mvumi Misheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, azma ya Serikali ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami iko pale pale na itatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa barabara hiyo itaendelea kuhudumiwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kufanya matengenezo ya aina mbalimbali kwa kiwango cha changarawe kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa wananchi wamezoea kabla ya barabara ya lami kujengwa huanza na upembuzi yakinifu: Mpaka sasa hivi hakuna hata dalili hizo: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuhakikishiaje wananchi wa Jimbo la Mtera kwamba upembuzi yakinifu utakaopelekea ujenzi wa lami ya barabara ile utaanza kufanyika?

Swali la pili, Naibu Waziri amejibu kwamba Serikali itaendelea kuitengeneza barabara ile kwa kiwango cha changarawe; barabara ile haijawahi kutengenezwa kwa kiwango hicho kwa muda mrefu. Je, kwa majibu hayo, Naibu Waziri anataka kutuhakikishia kwamba kwa maneno yake tu ya leo barabara ile imepandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, ni mfuatiliaji mahiri. Nami namhakikishia kwamba kutokana na juhudi zake anazozifanya, hatimaye hilo analolitaka litatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, naomba nimthibitishie kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi kwamba hii barabara iko chini ya TAMISEMI na itaendelea kuhudumiwa chini ya TAMISEMI kwa maana ya Halmashauri. Haijapandishwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusu upembuzi yakinifu, kwa kuwa kuna ahadi ambayo viongozi wetu waliitoa, kazi hiyo ya upembuzi yakinifu itaanza ili kuweza kuitekeleza ahadi hiyo na hatutaanza mwaka ujao wa fedha kwa sababu bajeti imepeleka vipaumbele katika maeneo yale ambayo Serikali tayari ilikuwa na *commitment*, na tunataka kwanza tumalize hizi *commitment*, baada ya kumaliza tutarudi kuhakikisha ahadi zote za Viongozi wetu zinatekelezwa, ikiwa ni pamoja na ahadi hii ya kupeleka lami kwenye barabara inayokwenda katika Hospitali ya Mvumi Misheni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nadhani hii *D by D* ianzie kwanza kwenu, halafu ndiyo mtuletee huku Bungeni, kwa sababu hata nyie maswali sasa hapa hatujajua nani anatakiwa kujibu. Kwa sababu kama ni barabara ya TAMISEMI, anapaswa ajibu Waziri anayehusika na TAMISEMI. Kwa sababu kama siyo ya Wizara ya Ujenzi, halafu yeye ndiyo anatakiwa kujibu swali, inaleta tabu kidogo. Kwa sababu yeye akiitolea ahadi, ahadi hiyo inabidi ifuatiliwe TAMISEMI. Kwa hiyo, nadhani mtusaidie hata huko mkae vizuri, maswali yaelekezwe kwenye Wizara inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kemi Lwota.

**MHE. KEMIREMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara ya Mkoa wa Mwanza hususan barabara ya Mwaloni iendayo kwenye Soko la Kimataifa la samaki, Mkuyuni, Kiseke, Nyamongolo Bulale na Kishiri. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutengeneza barabara hizi, zenye umuhimu wa kiuchumi kwenye Jimbo la Ilemela na Nyamagana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano; natumaini hizo ni barabara zako. Maana sasa kama ni za TAMISEMI tena! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoiongelea ni barabara yetu sote; sisi Ujenzi na

TAMISEMI; na kwa sasa iko chini ya TAMISEMI, lakini kazi tunaifanya kwa pamoja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika swali aliloliuliza kwamba tutafanya kazi kwa pamoja kati ya *TANROAD* Mkoa pamoja na wenzetu wa Halmashauri tuiangalie hii barabara ambayo inagusa eneo nyeti na muhimu la uvuvi ili tuweze kuiweka katika hali ambayo wavuvi wetu watapata fursa nzuri ya mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, tarehe 11/10/2014 ilikuwa siku ya Jumamosi saa 5.32; Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne wakiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, walizindua daraja la Mto Simiyu kule Maligisu na kuahidi kwamba mita 50 kuingia kwenye daraja na mita 50 kutoka kwenye daraja itawekewa lami. sasa nataka kujua, je, ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Richard Ndassa ni Mwalimu wangu. Naomba nimhakikishie kama ambavyo nimekuwa nikiongea naye kabla kwamba maungio haya ya daraja la Mto Simiyu kama ambavyo Viongozi wetu waliahidi, tutahakikisha tunayatekeleza. Naomba tu aendelee kutukumbusha, kwa kadri hapa ninavyoongea, wahusika wote kuanzia *TANROAD* Mkoa wa Simiyu, pamoja na Makao Makuu, wananisikia. Tuhakikishe hili daraja pamoja na barabara yake ambayo iliahidiwa, tuifanyie kazi kama ambavyo viongozi wetu waliahidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLELL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mkoa wa Arusha kwenda Chuo cha Mandela na hatimaye katika Vijiji vya Mlangarini, Nduruma na mpaka Bwawani Lusi ni barabara ambayo kwa muda mrefu imekuwa na kero. Tangu enzi za Elisa Molell akiwa Mbunge, Hatimaye Goodlucky Ole-Medeye mpaka sasa barabara hii kilio chake bado hakijasikikika. Je, Waziri anawaeleza nini wakazi wa vijiji hivi vya Mlangarini, Nduruma, Bwawani pamoja na Lusi kwamba barabara hii wataifikiria na kuweza kuijenga katika kiwango cha lami

na hasa ukizingatia Chuo hiki cha Nelson Mandela ni Chuo cha Kimataifa na kinatarajiwa kupokea wanafunzi wengi kutoka nchi mbalimbali? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri wazi kwamba tumesikia kilio cha Mheshimiwa Amina Molell na Chama cha Mapinduzi kwa utaratibu wake, Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa mikoa ambayo tumefanya *intervention* kubwa sana katika mradi wetu wa *CSP Project* ambao unafadhiliwa na *World Bank.* Sasa hivi Mji wa Arusha, Mbeya na baadhi ya miji, tumefanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii anayoizungumza Mheshimiwa Amina Molell, naomba niseme kwamba tumeisikia kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kwa kuwa pale kuna chuo kikubwa sana na vile vile hii ni ahadi yetu kwa wananchi hawa na lengo ni kuhakikisha lazima tunawahudumia. Serikali imesikia kilio hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 317

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kata ya Kizara**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Kata ya Kizara tangu uhuru haijawahi kuwa na mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini Kata hiyo itapatiwa mawasiliano ya simu?

**NAIBU WIZARA WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Kata ya Kizara haina mawasailiano ya uhakika ya simu. Kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ilikiingiza Kijiji cha Bombo-Majimoto kutoka katika Kata ya Kizara katika utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Vijijini wa Awamu ya Pili 'B'.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unaotekelezwa na Kampuni ya Simu ya *TIGO* kwa ruzuku ya Dola za Kimarekani 105,920, ulianza kutekelezwa tarehe 23 Mei, 2015. Hadi sasa *TIGO* wameshafanya *technical surveys* ya eneo la kujenga mnara na manunuzi ya eneo hilo ambapo mradi unategemewa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Vijiji vya Kilangangua, Kizara Kwemkole na Kwenkeyu vimo katika utekelezaji wa Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu ya miradi ya *Viettel* kwa maana ya *Hallotel* ambapo vijiji vinavyobaki vya Foroforo, Kiuzani na Mangunga-Mziya vitaingizwa katika miradi ya mawasiliano itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kutegemeana na upatikanaji wa fedha za mradi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kubwa mnazofanya za kusambaza mawasiliano nchi nzima.

Kwa kuwa tatizo la mawasiliano katika Jimbo la Korogwe Vijijini ilikuwa ni Kata nyingi hazina mawasiliano; na kwa kuwa Serikali hii ni sikivu; kuna Kata ambazo hazina mawasiliano kabisa, kwa mfano, Kata ya Dindira katika Kijiji cha Kwefingo, Kata ya Chekelee katika Kijiji cha Bagai, Kata ya Mkalamo katika Vijiji vya Kweisewa na Toronto, Bungani na Kata ya Kerenge katika Kijiji cha Makumba:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini vijiji hivi navyo vitajengewa minara ili nao wanufaike na Serikali hii ya Awamu ya Tano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani (Profesa Maji Marefu) kwa kunijulisha kwamba katika jibu langu la msingi la ujenzi wa mnara, ni kwamba kumbe tayari kazi imekamilika na umeme unawaka. Kilichobaki ni kutoa taarifa kwetu ili na sisi Wizara rekodi yetu tuweze kuirekebisha kuonesha kwamba umeme umewaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Profesa Maji Marefu na namhakikishia kwa kazi hii kubwa anayoifanya ya kufuatilia masuala haya na kutupa taarifa za uhakika katika maeneo mbalimbali ya eneo lake, kwa mfano: katika Kata ya Kerenge anafahamu mnara umejengwa katika Kijiji cha

Makumba, lakini vile vile Kata ya Dindira mnara umejengwa katika Kijiji cha Kwefingo ambacho ndiyo Makao Makuu ya Kata; anafahamu vile vile Kata ya Chekelei katika Kijiji cha Kwamkole nako mnara umejengwa; na mwisho Kata ya Mkalamo, Vijiji vya Kweisewa na Toronto Bungani, Minara imejengwa.

Hii yote hii ni kwa sababu ya juhudi zake za kufuatilia kwenye Makampuni yanayojenga minara; siyo Wizarani tu, bali na kwenye Makampuni yanayojenga minara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ngonyani na naomba ajaribu kuambukiza hiki kitu anachokifanya katika eneo lake kwa Waheshimiwa Wabunge wengine na hasa mimi mwenyewe. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Matatizo haya ya mawasiliano yaliyopo katika Jimbo la Korogwe Vijijini, yako pia katika Jimbo langu la Wilaya ya Mkuranga katika Kata ya Panzuo, katika Vijiji vya Mkuruwili, Kibesa na Kibuyuni, Kisegese, Chamgoi; Kata ya Kitomondo katika Kijiji cha Mpera na Mitandara na katika Kata ya Bupu katika Kijiji cha Mamdi Mkongo, Mamdi Mpera na hata kule Tundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Mheshimiwa Waziri aniambie, ni lini wananchi hawa wa vijiji nilivyovitaja katika Wilaya ya Mkuranga watapata mawasiliano ili na wao waweze kuendeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulega ameshaleta orodha ya hayo maeneo yote; kuanzia Kata ya Panzuo na hizo nyingine ambazo amezitaja katika Wizara yetu ili tuweze kuzifanyia kazi. Nami namhakikishia, orodha hiyo tumeipokea na tulishaiwasilisha kwenye Kampuni ya *Viettel* pamoja na *UCSAF* kwa maana ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili hatimaye watupe ratiba ya maeneo hayo yapangwe ratiba na bajeti kwa ajili ya kutekeleza kile ambacho Mheshimiwa Ulega anakipenda ili na wale wananchi wake waweze kunufaika na mawasiliano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Nachingwea tuna jumla ya Tarafa tano. Tarafa nne tayari zimeshafanikiwa kuwa na mitandao ya simu, lakini Tarafa moja ya Kilimarondo mpaka sasa hivi bado hamna mawasiliano ya uhakika na wako watu wa *TTCL* wameshafunga mitandao yao katika maeneo ya Kata ya Mbondo, Kegei pamoja na Kilimarondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo ninapozungumza ni mwaka wa tatu sasa, bado hawajawasha mitambo yao kwa ajili ya kutoa huduma. Naomba kuuliza swali. Nini mkakati wa Serikali juu ya kuhakikisha maeneo haya yanapata mawasiliano ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa namna anavyotupa moyo kuhusu uwekezaji uliofanywa na *TTCL* katika maeneo ya Jimbo lake. Namhakikishia kwamba kuanzia mwezi Septemba, *TTCL* itafanya mambo makubwa na nitahakikisha katika mambo haya makubwa yatakayofanywa kuanzia Septemba, 2016, eneo hili la Nachingwea ambapo tayari minara imeshajengwa litapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Mheshimiwa Profesa Maji Marefu la Korogwe Vijijini ni pacha kabisa na Jimbo la Mbulu Vijijini kutokana na hali ya kukosa mawasiliano. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano kwenye Kata ya Ari, Tumati, Mung'ahai, Ng'orati, Masieda, Endagi, Chani kule Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Massay alileta hiyo orodha na tuliongea na tena siyo na mimi tu, nilimpeleka na kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba kumhakikishia tena, siyo pale ofisini tu, hata na hapa. Sina tatizo, yeye aendelee tu kufuatilia, maana amefuatilia mara nne kuhusu suala hilo hilo, nami nampongeza sana kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tutatekeleza na tutafuatilia utekelezaji wa mawasiliano katika eneo hili la Mbulu Vijijini kama ambavyo tunafanya katika maeneo mengine na kwako nilikuahidi nitakuja. Siyo kwa

sababu hii tu, ni pamoja na ile barabara inayopitia Mbuyu wa Mjerumani mpaka lile eneo lako. Nilikuahidi na ninahakikisha nitalitekeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, Mbunge wa Nkansi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 318

**Ukamilishaji wa Skimu ya Lwafi**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Serikali imekwishatumia zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya Mradi wa Skimu ya Lwafi, lakini mradi huu haujawanufaisha kabisa wakulima zaidi ya 4000 kwa sababu haujakamilika:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha mradi huo ili uwe wa msaada kwa wakulima wa mpunga zaidi ya elfu nne?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi wa Tarafa ya Kilando kuhusu uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Lwafi, ilianza kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu husika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mnamo mwaka 2012, banio lilijengwa na mfereji mkuu wa urefu wa kilomita 1.6 ulichimbwa na kusakafiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mkopo kutoka Serikali ya Japan, Serikali inategemea kupeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mwezi huu Juni, 2016. Fedha hizo zitatumika kuchimba sehemu ya mfereji mkuu wenye urefu wa kilomita 16 na kusakafia na kujenga maumbo ya maji ndani ya mfereji huo. Hatua hiyo itawezesha wakulima wa mpunga katika skimu hiyo kunufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kama Serikali ipo tayari kupeleke pesa hizo, lakini nataka kujua ni shilingi ngapi zitapelekwa kwa ajili ya kumalizia huo mradi wa Skimu ya Lwafi? Nataka kujua kiasi cha pesa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha itakayopelekwa kule ni shilingi milioni 550 na fedha hii inatolewa na Serikali ya Japan na tayari taratibu za kuipeleka hiyo fedha zimeshafanyika ila kumekuwa na matatizo kidogo kupanua ile *item* ya kulipia kwa upande wa Halmashauri, ndiyo Serikali inaendelea kupanua. Fedha hiyo ipo tayari na wakati wowote itaingia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dotto Biteko.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hali iliyopo Lwafi inafanana sana na hali iliyopo na mpango wa Wilaya ya Bukombe ambapo skimu ya umwagiliaji ilijengwa, iliyokuwa inagharimu shilingi milioni 606, lakini fedha ambazo zimeshatoka ni asilimia 58 peke yake. Skimu hiyo ilikuwa inakusudiwa kuhudumia Vijiji vya Kasozi, Nampangwe pamoja na Kijiji cha Msonga na hekta 100 zingeweza kuhudumiwa na skimu hii. Mpaka tunavyozungumza hapa, mradi huo umesimama: Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Nampangwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba skimu hiyo haijakamilika na kwamba fedha iliyolipwa ni asilimia 58 tu. Namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tumeamua kwanza kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea; na kwa sasa tupo vizuri. Tume ya Umwagiliaji imeshaundwa na ipo sasa hivi inajipanga, kwa hiyo, sasa hivi tutakuwa na mfumo mzuri wa kuhakikisha miradi hii inakamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Matembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Miradi ya maji iliyopangwa kutelekezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini ya ukarabati wa miundombinu ya visima ya Sagara, Mdilu, Ihanuda na Mwasawiya pamoja na ile inayotumia pampu za mkono ya Vijiji vya Muhamo, Mkimbii, Mwanyonye, Mitula, Mwakiti, Ndugwire, Gauri na Kinyeto haijatekelezwa mpaka sasa na hii ni kutokana na ukosefu wa fedha:-

Swali; ni lini na wakati gani fedha zitaletwa kukamilisha miradi hii? Je, ni lini Serikali itawatua ndoo wanawake wa Mkoa wa Singida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose swali la nyongeza, unauliza moja tu. Kwa hiyo, chagua kati ya hayo maswali, unalotaka ujibiwe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE:** Je, ni lini na wakati gani fedha zitaletwa kukamilisha miradi hii? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya visima Singida, nimeeleza katika Bunge hili kwamba kuanzia sasa hivi Serikali haitapeleka fedha kwenye miradi ya maji kabla miradi haijatekelezwa. Kinachotakiwa ni kwamba lazima kwanza ulete *certificate* ili tuwasilishe Hazina kuomba fedha tuweze kuzileta.

Swali lake, ni lini fedha zitaletwa? Fedha tutapeleka kulingana na upatikanaji wa fedha katika Serikali na nina hakika kwamba mwaka wa fedha unaokuja, akituletea *certificate* kuhusu hivi visima, kwa vyovyote vile fedha tutapeleka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega. Mheshimiwa Chegeni, nililetewa ujumbe hapa kwamba swali lako umeagiza uuliziwe kwa niaba. Haya, endelea Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza Kiti kimekufiti vizuri sana, nakupongeza kwa hilo. Makofi hayo yanaashiria kwamba kazi ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu namba 319 pamoja na nia njema ya kutaka kuuliziwa na mtu mwingine, sasa lijibiwe. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 319

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Busega**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu unaanzia Wilaya ya Busega na tayari mipango pamoja na fedha ya kuanza kutekeleza mradi imeshapatikana:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji safi kutoka Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Simiyu katika Miji Mikuu ya Wilaya za Bariadi, Maswa, Meatu, Itilima na Busega pamoja na vijiji vilivyopo umbali wa kilomita 12, kando ya bomba kuu. Tayari Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa mkabrasha ya zabuni ameajiriwa. Gharama za utekelezaji wa mradi mzima zinakadiriwa kuwa kiasi cha *Euro* milioni 313 na mradi huu utatekelezwa katika awamu mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza itagharimu kiasi cha *Euro* milioni 105 na itahusisha kufikisha maji katika miji mikuu ya Wilaya za Bariadi, Itilima na Busega pamoja na vijiji vilivyo kando ya bomba kuu. Hadi hivi sasa Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya *KFW* imechangia kiasi cha Euro milioni 25 na kiasi kilichobaki cha *Euro* milioni 80 kinatarajiwa kupatikana kutoka Mfuko wa *Green Climate Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017 na utachukua miaka miwili hadi kukamilika. Kwa sasa mtaalam mshauri anaendelea kufanya usanifu wa tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika maeneo ya mradi huo. Kazi hiyo itakamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya mradi itafikisha maji katika Miji ya Mwanhuzi na Maswa kwa gharama ya *Euro* milioni 208. Fedha hizi pia zinatarajiwa kutoka *Green Climate Fund*. Miradi hii ikikamilika, inatarajiwa kunufaisha watu zaidi ya 834,204.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kwa Serikali yetu kwa mpango mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu kwa kweli ni mradi ambao una tija kubwa sana kwa wananchi wa maeneo husika katika Wilaya ya Busega, Wilaya ya Itilima, Bariadi, Maswa na Meatu. Kwa kuwa mradi huu utakapopita vijiji ambavyo vipo umbali wa kilomita 12, kushoto na kulia mwa bomba kuu, vitapata huduma ya maji: Je, Serikali ina mpango gani kwa vijiji ambavyo vipo

nje ya mradi huu kupatiwa maji ili waweze kunufaika na mradi wa namna hii? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Ziwa Victoria lina maji mengi sana na mikoa mingi ina matatizo ya maji, kwa nini Serikali isiwe na mpango mwingine kabambe; baada ya Mkoa wa Simiyu kupata maji, basi Mkoa wa Singida na wenyewe upate maji na mpaka Dodoma nao waweze kupata maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa pongezi; lakini pili, vijiji vinavyotarajiwa kunufaika na mradi huu ambavyo vipo umbali wa kilomita 12 kutoka katikati ya bomba ni vijiji 223.

Swali lake namba moja ameuliza, vijiji ambavyo vipo nje ya zile kilomita 12; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya mradi kukamilika huwa tuna utaratibu wa kuendelea kutoa fedha kwenye mamlaka zilizo karibu na hilo bomba ili ziweze kuendeleza kupeleka maji kwenye maeneo ambayo hayakupitiwa na huo mradi. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo kama ambavyo tumeshaendelea kufanya kwenye mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga.

Swali la pili, Ziwa Victoria lina maji mengi; ni kweli lina maji mengi. Kuna utaratibu gani wa kupeleka maji kwenye maeneo ambayo hayajapata maji ikiwemo pamoja na Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tayari tuna mradi tumepata Dola milioni 265 na mwaka wa fedha unaokuja tunasaini mkataba kwa ajili ya kupeleka maji ya Ziwa Viktoria, Nzega, Mkoa wa Tabora hadi Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumesema kwamba sasa hivi tutaanza kufanya utafiti, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kupeleka maji pia katika Mkoa wa Singida ambao ni mkoa kame na hauna maji ya kutosheleza kule chini. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya tafiti ili kuhakikisha kwamba maji yanawafikia wananchi wote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Wananchi wa Vijiji vya Kitulila, Mwatola, Luponde, Njomlole, Lusitu na Uwemba walichanga fedha kama asilimia 10 ya mradi wa maji ya mtiririko kutoka katika milima ya Igongwi

Ludewa: Je, ni lini mradi huu sasa utaanza kutekelezwa ili wananchi hawa waweze kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulivyoanza mradi wa *WSDP* tulisema kwamba mradi huu ni shirikishi na wananchi ilibidi wachangie, lakini sasa tumeamua kwamba fedha zile ambazo wanachangia wananchi hazitatumika wa kujenga miradi ila watazitumia katika kuiendesha miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, asilimia ambayo vijiji wameweza kujenga, watatumia katika kuendesha ile miradi itakapokamilika. Lini miradi ile itaanza? Tumetoa *program* na bajeti tumepitisha, tumeeleza utaratibu. Kwa hiyo, kila Halmashauri ilileta vijiji vya kipaumbele, kwa hiyo, naamini vijiji anavyovisema, Halmashauri yake iliviweka kwenye kipaumbele, tutaanza katika mwaka wa fedha wa 2016 /2017. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Busega linafanana na tatizo la Mkoa wa Tabora, hususan Tabora Manispaa; na kwa kuwa tuna bwawa la Kazima ambalo kina chake ni kifupi: Je, Serikali ipo tayari sasa kukarabati bwawa hilo ili tuweze kupunguza tatizo la maji Mkoa wa Tabora hususan Tabora Manispaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la Kazima lilijengwa mwaka 1946 na bwawa hili lilijengwa na watu wa reli kwa ajili ya kupata maji ya kupoza *engine* zile ambazo zilikuwa zinatumia mkaa. Mwaka 1990 matumizi yalibadilika baada ya kupata *engine* ambazo zinatumia *diesel,* kwa hiyo, ikaamuliwa bwawa hili liwe linatumika kwa ajili ya maji ya kunywa. Sasa hivi linamilikiwa na Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Tabora (*TUWASA)* na linazalisha lita milioni 1,400 ya maji safi na salama kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka imeomba shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuimarisha lile tuta kwa sababu mwaka huu maji yalijaa sana, lakini pia lipo shirika linalohudumia maeneo ya *Lake Tanganyika.* Mamlaka wameomba ili waweze kulikarabati lile bwawa liendelee kuhimili kuweka maji mengi na kuendelea kuwahudumia wananchi wa Tabora. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwanne nikuhakikishie kwamba suala hili linafanyiwa kazi kuhakikisha kwamba bwawa hili linakarabitiwa.

**MHE. NDAKI M. MASHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa mradi wa maji kutoka Busega, Bariadi, Itilima hata Maswa Mjini unaishia Maswa Mjini kwa maana ya Jimbo la Maswa Mashariki na kwa kuwa Wizara Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nimewashauri kwa Jimbo la Maswa Magharibi tuunganishwe na mradi wa maji unaotoka Ngudu, Malya, kuja Malampaka. Je, Serikali ipo tayari sasa kuchukua ushauri wangu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tunaupokea ushauri, tutaufanyia kazi, lakini maji yatatoka wapi? Itategemea na utafiti wa wataalam kuangalia sehemu ambayo itakuwa ni rahisi kuyafikisha maji. Kwa hiyo, niseme tu kwamba ushauri wake tunaupokea na lengo siyo kupeleka maji mijini tu, hapana. Kama nilivyosema katika jibu nililojibu muda mfupi uliopita ni kwamba tutakuwa tunaendelea kutenga fedha, kama maji yanatosheleza, yaendelee hata nje ya miji.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

Na. 320

**Mgogoro Kati ya Wananchi na Jeshi**
**Kata ya Misunkumilo**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (K.n.y. MHE. RHODA E. KUNCHELA)** aliuliza:-

Kumekuwa na sintofahamu katika eneo la Kata ya Misunkumilo, Wilaya ya Mpanda Mjini, Wanajeshi wanadai eneo hilo ni la Jeshi, lakini makazi ya wananchi yalitangulia na wana hati ya maeneo yao:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutatua jambo hili ikiwa Jeshi limewakuta wananchi katika eneo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu za kistratejia, JWTZ lilipewa eneo la Misunkumilo lililopo Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda mwaka 1985

lenye ukubwa wa hekta 3195. Serikali ililipa fidia kwa wananchi waliokuwepo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1992 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilihamisha kombania yake kutoka katika eneo hilo ila eneo alikabidhiwa Mkuu wa Wilaya kwa uangalizi. Kutokana na sababu za kiusalama hasa ukanda wa Ziwa Tanganyika, imebidi Jeshi lirejee kwenye sehemu hiyo tena. Hata hivyo, sehemu ya eneo hili sasa limevamiwa na kupangiwa matumizi mengine na uongozi wa Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Novemba, 2015 kilifanyika kikao cha pamoja kati ya JWTZ na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Katavi. Maamuzi yaliyofikiwa katika kikao hicho ni kulipima upya eneo hilo kwa kuzingatia maendeleo yaliyopo, lakini vile vile na mahitaji ya JWTZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi eneo hili litapungua kutoka ekari 3,195 za awali hadi 2,235. Zoezi la kupima upya litakuwa shirikishi na litatekelezwa mara fedha zitakapopatikana katika mwaka wa fedha wa 2016/2017. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanjelwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, katika mgodi wa JPM ambao uko katika Kata ya Mpanda Hoteli ilikuwa ni sehemu ambayo imewekwa mizinga ile ya kijeshi; lakini hapo hapo katika mgodi huo wa JPM kwa sababu wengi ni wawekezaji wageni, lakini wananchi wa mahali pale wanapata shida sana. Naomba Serikali iweze kutoa tamko kwa sababu wananchi hao wananyanyaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mimi natoka Mbeya, lakini pale Mbeya sehemu ya Mbalizi kuna Jeshi la Wananchi ambao wako pale na liko jirani sana na wananchi hususan Kata ya Iwindi na Utengule, Usongwe. Sasa nina wasiwasi kwamba lisije likatokea jambo ambalo lilitokea Mbagala. Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi hawa ambao wanaweza wakapata madhara kama ya Mbagala? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa anazungumzia unyanyasaji aliouita unyanyasaji ambao unafanywa na Jeshi la Wananchi kwenye mgodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe hili jambo tulifanyie utafiti na tulichunguze uhalisia wake. Baada ya hapo ndiyo tutakapoweza kutoa tamko la Serikali. Sehemu ya pili, swali lake la pili kuhusiana na Mbeya ni kweli, baada ya kutokea matatizo yale ambayo yalitokea Mbagala, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba inadhibiti matatizo kama yale yasijitokeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwahakikishia tu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba hatutarajii matatizo kama haya yajitokeze kwa sababu Serikali imechukua hatua madhubuti. Hata hivyo, hatutalidharau jambo hili ambalo amelizungumza Mheshimiwa Mbunge nalo pia tutalichukua, tulifuatilie kwa kina tuone kama kuna kasoro tuweze kuzifanyia kazi na kuzirekebisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alikuwa anajibu kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Kwa hiyo, nadhani maswali ya nyongeza yatakuwa yanamtosha kwa leo.

Tuendelee. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 321

**Utaratibu wa Serikali Kutoza Kodi ya *Motor Vehicle* kwa Magari Mabovu**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wizara ya Fedha katika juhudi zake za kukusanya mapato ya Serikali, imeweka Sheria ya Kukusanya Kodi ya Magari inayoitwa *Motor Vehicle* au *Road License*. Kodi hiyo imekuwa ikilalamikiwa sana na wananchi kwa kuwa imekuwa ikidaiwa hata kwa magari mabovu au ambayo yamepaki kwa muda wote bila kujali kipindi ambacho gari lilikaa bila kufanya kazi:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuitazama upya sheria hii?

(b) Kwa kuwa kodi hudaiwa hata kipindi ambacho gari halifanyi kazi: Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo inawaibia wananchi wake?

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikwembe naomba utulie. Mwenye swali aliacha maagizo nani amwulizie swali lake. Ni sawa, lakini ameacha maagizo Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa amuulizie. Usigombane, inakuwa siyo tabia nzuri.

Tuendelee Waheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya *Motor vehicle Annual License* inasimamiwa chini ya Sheria ya *Road Traffic Act,* 1973 pamoja na kanuni zake *(The Road Traffic* na *Motor Vehicle Registration Regulations)*. Sheria hii imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kulingana na mahitaji ya wakati husika. Kodi hii ni moja ya kodi zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kutumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini na kutoa huduma mbalimbali. Hivyo hatuwaibii wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *The Road Traffic Motor Vehicle Registration Regulations* ya mwaka 2001, Sura ya Pili, Kifungu cha (4) na (5) hakuna msamaha wa leseni ya gari kwa mtu yeyote na inataka ada hiyo kulipwa kila mwaka tangu gari husika liliposajiliwa. Hivyo, sheria haitoi unafuu wowote kwa gari lililosimama kwa muda mrefu bila kutembea barabarani. Ni kweli utekelezaji wa sheria hii unaleta adha kwa wamiliki wa magari na hasa pale ambapo kuna ushahidi wa kutosha kwamba gari husika limesimama kwa muda mrefu na kwa sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa adha hii, Mamlaka ya Mapato imeanza mchakato wa kuboresha sheria hii ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuhudumia wamiliki wa magari ambayo yatakuwa yamesimama kwa kipindi kirefu bila kutembea barabarani kwa sababu za msingi. Aidha, baada ya taratibu zote kukamilika, mapendekezo ya mabadiliko ya sheria hii yataletwa Bungeni ili kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata, swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Serikali ya Awamu ya Tano katika matendo yake imeonekana inasimamia haki. Nataka

kujua kama pato la kodi hii Serikalini kwa magari yaliyosimama kwa muda mrefu kwa sababu za msingi, lina tofauti yoyote na pato analolipata mwananchi au mtumishi hewa kutoka Serikalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni ushauri. Kwa kuwa magari yanayotozwa kodi hii hutumia mafuta na kwa kuwa kodi hii imekuwa na adha katika ukusanyaji wake na ni kero pia kwa wananchi: Je, Serikali inapokea ushauri kwamba, kodi hii ihamishiwe kwenye mafuta ili kurahisisha ukusanyaji wake na kuondoa kero kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kodi hizi hutozwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge letu Tukufu. Kwa hiyo, kuifananisha na watumishi hewa siyo sahihi kabisa na ndiyo maana nimesema Serikali ina nia na imeanza maboresho ya sheria hii ili kuweza kuondokana na adha hii wanayoipata watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuifananisha kwa sababu ni ngumu kwa sababu ya jiografia ya nchi yetu. Huwezi tu kusema gari hii imesimama bila kujiridhisha kweli imesimama. Kama ilitolewa mjini na ikapelekwa Vijiji ambavyo hatuwezi kuvifikia, inakuwa ni tatizo kusema gari hili limesimama. Ndiyo maana nasema, naomba tuvute subira, tutakapoleta *Finance Bill* ya mwaka huu 2016/2017 anachokipendekeza Mheshimiwa Mbunge kitaonekana na adha hii itaondoka kabisa wala haitakuwepo tena kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa pamoja na upungufu uliopo katika kodi hii, lakini pia baadhi ya wananchi ambao sio waaminifu walikuwa wanatumia mwanya huo kutengeneza *sticker* ambazo ni feki: Je, Serikali ina mpango gani wa kuja na *sticker* madhubuti ambazo siyo rahisi kufojiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wapo wananchi ambao wanatenda vitendo viovu vya kufoji *sticker* hizi. Kama nilivyosema, lakini naomba pia tufahamu kwanza Waheshimiwa Wabunge, katika sehemu ambako tumeboresha kwa kiasi kikubwa ni utoaji wa *sticker* hizi ambapo kwa sasa hivi mwananchi yeyote anaweza kulipia gari yake popote alipo na akaenda kuchukua risiti yake katika Ofisi zetu za Mamlaka ya Mapato popote pale alipo huku akiwa amepewa *control number.* Kwa hiyo,

tumeweza kutoka katika *manual work* na sasa tunatumia teknolojia katika kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maboresho hayo, kama nilivyosema, tusubiri *Finance Bill* itakapokuja, tutaona sasa kutakuwa hakuna mkono wa mtu yeyote kuingia katika ukusanyaji na utoaji wa *sticker* hizi kwa sababu itakuwa ni mfumo wa *automatic* ambao hakuna yeyote atakayeweza kuuingilia na kuweza kutoa *sticker* ambazo ni feki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 322

**Ahadi ya Serikali Kongeza Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Sekta ya Utalii ni Sekta inayotegemewa kuliingiza Taifa mapato kwa sababu ya vivutio vingi tulivyojaliwa Tanzania:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza ahadi iliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2016 - 2020 katika kuongeza bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii?

(b) Je, ni nini mkakati wa Serikali kukiimarisha Chuo cha Utalii ili kutoa mafunzo ya Hoteli na Utalii katika ngazi ya Stashahada ili kuongeza ubora wa Watumishi wa huduma za ukarimu na utalii?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka mazingira bora ya kuwezesha vijana kuanzisha makampuni ya kutembeza watalii katika maeneo mbalimbali ya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2016 -2020, katika Ibara ya 29(c) inaainisha azma ya Chama cha Mapinduzi kusimamia Serikali katika utekelezaji wa mikakati ya kukuza utalii nchini kwa kuhakikisha kwamba bajeti ya Sekta ya Utalii inaongezeka ili kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati huo, Wizara yangu kupitia Bodi ya Utalii na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania imetenga jumla ya sh. 2,730,188,676/= kwa ajili ya shughuli za utangazaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017, hii ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.7 ikilinganishwa na mwaka 2015/2016. Serikali itaendelea kuboresha utekelezaji wa ahadi hii kwa kushirikisha pia wadau mbalimbali wa maendeleo na vyanzo vingine kama inavyoainishwa na mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali katika kukiimarisha Chuo cha Utalii katika Kampasi zake zote tatu za Bustani, iliyoko Dar es Salaam; ya Temeke iliyoko Dar es Salaam pia na ya Arusha. Ni pamoja na kuongeza idadi na umahiri wa wakufunzi, kuboresha upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kuboresha miundombinu ya chuo katika kampasi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya hivi karibuni Chuo cha Utalii kitaboresha utoaji wa mafunzo katika Tasnia ya Ukarimu *(Hospitality)* na Utalii *(Tourism)* katika ngazi ya Shahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Chuo cha Utalii kwa kushirikiana na Chuo cha *Vancouver Island University* cha Canada kupitia Mradi wa *ISTEP* chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kitaanzisha mafunzo ya uongozi katika ngazi ya Shahada kuanzia mwezi Septemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa miundombinu, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2016/2017 ili kukamilisha ujenzi wa jengo la Utalii *(Utalii House) Phase II* katika Kampasi ya Bustani ya Chuo cha Utalii, Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira bora ya kuwezesha vijana kuanzisha makampuni ya kutembeza watalii katika maeneo mbalimbali ya utalii; Serikali itaendelea kwa msisitizo zaidi kushirikisha sekta binafsi ili kuwashauri vijana wajiunge katika vikundi na kuwapa elimu ili waanzishe na kushiriki kwa tija zaidi katika biashara hii kwa maslahi yao na kwa maslahi ya Taifa. Serikali pia itapitia masharti yote yaliyopo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ili kuona kama kutakuwa na uhitaji wa kuyafanya masharti hayo kuwa rafiki zaidi kwa vijana wenye nia thabiti ya kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa Taifa kupitia shughuli za uongozaji watalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangoye, swali la nyongeza.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa

kuongeza Vyuo vya Utalii katika Mikoa mingine ya Tanzania hasa katika ngazi ya shahada? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Mwanza una makumbusho mbalimbali ya kihistoria yakiwemo ya Kageye na makumbusho ya kabila la Kisukuma yaliyopo Bujola Wilayani Magu, ambayo yamekuwa yakipoteza umaarufu wake kadri miaka inavyoongezeka. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba umaarufu huu wa makumbusho haya unaongezeka ili kuiwezesha Wilaya ya Magu kupata kipato kupitia utalii hasa tukizingatia kwamba Wilaya hii imekuwa na mapato madogo kiasi kwamba, imekuwa haikidhi haja ya utoaji wa asilimia kumi ya mapato yake kwa ajili ya vijana na wanawake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza la kuongeza vyuo vya utalii na hasa katika ngazi ya shahada, napenda kutoa maelezo ambayo ndani yake kuna majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, Serikali itaelekeza nguvu zake zaidi kwa sasa katika kuimarisha vyuo vilivyopo, vile ambavyo nimevitaja katika *campus* tatu, mbili zikiwa Dar es Salaam na moja ikiwa pale Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunazingatia kuongeza vyuo zaidi, tutazingatia pia ukweli kwamba kitaalam na hasa unapozungumzia kuongeza mafunzo hayo katika ngazi ya shahada ili wahitimu wenye ngazi ya Shahada waweze kufanya kazi sawasawa na yenye tija, unahitaji zaidi kuwa na wataalam katika ngazi ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaelekeza nguvu zetu zaidi kwa wataalam wa ngazi ya kati sambamba na kuangalia uwiano kati ya wale wahitimu wanaohitimu katika vyuo vya kati ili tuweze kuboresha zaidi utendaji wa wale ambao watakuwa wamehitimu katika ngazi ya shahada hapo baadaye, lakini kwa sasa hivi tuelekeze nguvu nyingi zaidi katika kuzalisha wataalam katika ngazi ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la makumbusho yaliyoko katika Mkoa wa Mwanza na umaarufu wake unaoendelea kupungua, namwomba Mheshimiwa Mbunge arejee majibu ya maswali yaliyotangulia hapo awali. Hata hivyo, nitarudia pia kwa ufupi kwamba, hivi sasa mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni kwenda katika kila Halmashauri ya Wilaya nchini na kuorodhesha aina zote za vivutio vya utalii ikiwemo makumbusho mbalimbali ili tuweze kupanga vizuri zaidi namna ya kuweza kuvitunza vile vilivyopo katika hali iliyopo, kuviboresha na kuweza kuvifanya

viweze kuchangia vizuri katika uchumi wa Taifa kwa kadri ambavyo tutaweza kuvitangaza zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ni Wilaya yenye vivutio vingi vya kitalii na vijana wa Lushoto wanafanya kazi ile kwa mazoea. Je, ni lini Serikali itafungua Chuo cha Kitalii ili kuwajengea uwezo vijana wa Lushoto ili wasifanye kazi ile kwa mazoea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza vijana wa Lushoto kwa moyo wao wa kujitokeza kupenda kufanya kazi katika eneo hili, kwa sababu kupitia kwao, tutaweza kufanya ajira kwa vijana ikawa imepata mchango mkubwa sana kupitia Sekta ya Utalii na kupitia kwao tunaweza kuchangia vizuri zaidi uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufanya kazi kwa mazoea na mahitaji ya kupata mafunzo, kwanza nipate takwimu kwa sababu kwa sasa hivi Mheshimiwa Mbunge ametoa maombi ambayo ni ya jumla, nimtake sasa tuweze kushirikiana, nione kwamba kwenye eneo la Lushoto lile kuna vijana wangapi ambao wamejitokeza kupendelea kuingia katika fani hii. Kwa sababu ninachoamini ni kwamba vyuo tulivyonavyo bado havijaelemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizopo mpaka sasa hivi, vyuo tulivyonavyo bado vina uhitaji wa wanafunzi; lakini kama itajitokeza kwamba vyuo vinalemewa na kuna uhitaji wa kuongeza vyuo vingine, au kuboresha mazingira ya vyuo vilivyopo ili viweze kupokea wanafunzi zaidi, basi Serikali itaweza kuchukua hatua muafaka ili kila mmoja mwenye nia na kiu ya kujiunga kwenye mafunzo yatakayompelekea kuwa na taaluma muhimu ya kushiriki vizuri zaidi kwenye Sekta hii ya Utalii aweze kufanya hivyo bila mashaka yoyote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa nchi yetu kiutalii na kitakwimu tunaambiwa ni nchi ya pili kwa kuwa na vivutio baada ya Brazil na ili kunufaika zaidi na utalii ambao tunaambiwa pia kitakwimu ndiyo sekta zinazoongoza kwa kuingiza fedha za Kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusudi kuiwezesha Bodi ya Utalii Tanzania kufanya *promotion* na *advertisement* kwa kiwango cha kuridhisha na hivyo kuongeza idadi ya watalii; je, Serikali iko tayari sasa kuunda chombo maalum ambacho kitasimamia ile *Tourism Development Levy* kusudi kuiwezesha *TTB* kufanya *promotion* na *advertisement* kwa kiwango kikubwa ili kuvutia watalii wa kutosha na hivyo kuongeza mapato ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na nafikiri hapa anatukumbusha tu; kama ambavyo nimesema mara nyingi, nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii; na ni ya pili baada tu ya Brazil. Kuhusu suala la *Tourism Development Levy (TDL)* namna ambavyo inaweza kuchangia zaidi na inavyoweza kusaidia zaidi Bodi ya Utalii, *(Tanzania Tourism Board)* kufanya majukumu yake vizuri zaidi na wazo la kuanzishwa kwa chombo kingine tena cha kuweza kusimamia *TDL*, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi, suala la *(Tourism Develeopment Levy - TDL)* kama lilivyo, halina matatizo yanayohitaji kuanzishwa kwa chombo kingine kusimamia. Tunahitaji kuboresha vizuri zaidi usimamizi kupitia vyombo vilivyopo chini ya Serikali hivi sasa, lakini ni kweli kwamba tunakwenda sasa kujipanga vizuri zaidi ili mapato yanayopatikana kutokana na *Tourism Develepment Levy* yaweze kusaidia zaidi Bodi ya Utalii kutimiza majukumu yake ambayo kwa kiwango kikubwa ni kutangaza utalii ndani na nje ya mipaka ya nchi hii kwa ajili ya kuboresha mapato ya Taifa kupitia Sekta ya Utalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim Khamis, Mbunge wa Mwanakwerekwe; swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir.

Na. 323

**Madai ya Kuuzwa Kisiwa cha Shungimbili**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR (K.n.y. MHE. ALI SALIM KHAMIS)** aliuliza:-

Kisiwa cha Shungimbili kilichopo Wilaya ya Mafia kinamilikiwa na mwekezaji ambaye amekibadilisha jina na kukiita Thanda, mmiliki wake ni Kampuni ya Utalii ya *Zululand* ya Afrika Kusini. Aidha, kuna madai kuwa kisiwa hicho kimeuzwa kwa mwekezaji huyo; kwenye kisiwa hicho kuna hoteli yenye hadhi ya dunia na ndicho kisiwa ghali duniani kuishi kwani kwa siku ni *USD 10,000* na ili upate chumba ni lazima ufanye *booking* kwa muda usiopungua siku saba:-

(a) Kama kisiwa hicho kimeuzwa: Je, kimeuzwa shilingi ngapi na hoteli hiyo inalipa kodi kiasi gani kwa Serikali?

(b) Je, Wizara ya Maliasili na Utalii inashirikiana vipi na Wizara ya Utalii Zanzibar hasa ukizingatia Wizara ya Mambo ya Nje ni ya Muungano katika Mikataba ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA MALISILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Salimu Khamisi, Mbunge wa Mwanakwerekwe, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kisiwa cha Shungimbili ni moja ya visiwa vitatu vilivyopo katika Wilaya ya Mafia. Visiwa hivyo vitatu na vingine 12 vinafanya jumla ya visiwa 15 ambavyo ni maeneo tengefu yanayosimamiwa na Taasisi ya Hifadhi za Habari na maeneo tengefu yaliyopo nchini, chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Kimsingi Taasisi hii ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 29 ya mwaka 1994 ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia maeneo yote yaliyotangazwa kuwa hifadhi za habari *(Marine Parks)* na maeneo tengefu ya bahari *(marine reserves)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisiwa cha Shungimbili hakijauzwa na baada yake kimeingizwa katika uwekezaji kupitia Kampuni ya *Thanda Tanzania Limited* inayojenga *Lodge* ya kitalii ikiwa ni majawapo ya mipango ya Taasisi ya *MPRU* ya kuimarisha uwekezaji katika maeneo inayosimamia ili kuongeza mapato ya Serikali na kutekeleza Sera ya Utalii ya mwaka 1999. Aidha, uwekezaji huo umepita taratibu zote za Serikali na utakapokamilika mwekezaji atatekeleza wajibu wake ikiwemo kulipia tozo zote kwa mamlaka zinazohusika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, ndiyo yenye dhamana ya kuingia mikataba yote ya Kimataifa, yenye maslahi kwa nchi nzima Bara na Visiwani. Hata hivyo, pamoja na kwamba nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 haijaorodhesha Sekta ya Utalii kama moja ya maeneo ya Muungano, haijazuia Wizara zinazosimamia Sekta ya Utalii kutoka pande hizi mbili kuendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano unaozungumziwa unajumuisha maeneo ya utangazaji wa vivutio vya Tanzania

Kimataifa kama nchi moja, utayarishaji taarifa na ujenzi wa mifumo imara ya ukusanyaji wa takwimu kupitia Kamati inayojulikana kama *The Steering Committee of the Tanzania Tourism Sector Survey* na mikutano mbalimbali ya ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na ile ya uwezeshaji utalii *(Tourism Facilitation Committee)* ya wadau wa utalii. Wizara yangu itaendelea kudumisha na kuuboresha uhusiano huu kwa sababu mtawanyiko wa vivutio vya utalii unagusa Tanzania kama nchi moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tahir, swali la nyongeza.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi, lakini nina maswali madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kuliambia Bunge hili kwamba suala la Kampuni ya *Zululand* kwamba ni ya Afrika Kusini ni kauli ya upotoshwaji kwamba inamiliki Kisiwa hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya utalii Zanzibar na ile ya Muungano, wanashirikianaje katika suala zima la utalii katika ulimwengu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli kama nilivyofafanua kwenye jibu langu la msingi kwamba Kisiwa cha Shungimbili na kazi inayofanyika hivi sasa pale, kwa ujenzi wa ile hoteli ya Kitalii, ile *lodge;* inaendelea kufanyika chini ya *MPRU* ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo na Uvuvi, kazi hiyo itakapokamilika, itakapoingia sasa kwenye masuala ya uwekezaji yenyewe; ya uendeshaji wa biashara yenyewe ya hoteli; pale sasa ndiyo Wizara ya Maliasili na Utalii inapoingia, watakapokuja sasa kuomba Leseni ya Biashara ya Utalii ambapo sasa watalazimika kuomba leseni hiyo chini ya chombo chetu cha *Tanzania Tourism Licencing Board*. Pale tutaweza sasa kutoa hiyo leseni, ikiwa watakidhi vigezo vyote ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano kati ya Bara na Visiwani, ni kama nilivyojibu kwenye swali la msingi na niliorodhesha masuala kadhaa ambayo tunayafanya kwa kushirikiana baina ya pande zetu zote mbili za utalii. Kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge mwuliza swali pamoja na Wabunge wengine, nimesema ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano, unajumuisha maeneo ya utangazaji wa vivutio vya Tanzania Kimataifa kama nchi moja, utayarishaji taarifa na ujenzi wa mfumo imara wa ukusanyaji wa takwimu ambapo takwimu hizo sasa ndiyo zinatumika Kimataifa kwa ajili ya kuifahamu vizuri zaidi nchi yetu na masuala yanayohusiana na utalii, kwa sababu ni takwimu zinazohusiana na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimetaja hayo mawili miongoni mwa manne ambayo nimekwishayataja, lakini mtu anaweza kurejea kwenye jibu langu la msingi kwamba hayo ndiyo maeneo ambayo tunafanya ushirikiano au mashirikiano baina ya pande hizi mbili za Muungano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Ningependa tu kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwa kuwa hoteli hizi ambazo ni maalum sana, ambazo zinaitwa 'za Kimataifa', zinazojengwa kwenye maeneo maalum, zimekuwa zikichukua ajira za wafanyakazi wengi kutoka nje, zile ambazo ni muhimu sana na kuwaacha wazawa wakifanya kazi zile ndogo ndogo kwenye hayo mahoteli makubwa. Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha kwamba nafasi zile kubwa zinachukuliwa na wazawa kuliko wafanyakazi kutoka nje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa ufupi kabisa! Ukweli ni kwamba mfanyabiashara anapotafuta mtu wa kumwajiri ili aweze kutoa huduma katika eneo lake la biashara, lazima atakuwa anatafuta mtu ambaye atamwezesha kupata tija katika biashara yake. Kwa hiyo, hilo linakuwa ni suala la ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeliona jambo hili kwamba kwa upande wa nchi yetu, tunao upungufu kwa kiwango fulani juu ya kuweza kushindana katika masoko haya ambayo yanahusisha ushindani wa Kimataifa. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo tutaifanya ni ile ambayo tunaboresha zaidi Vyuo vyetu ili tuboreshe zaidi wananchi wetu, waingie, wajifunze; lakini siyo kujifunza tu darasani, wakitoka pia waweze kufanya kama walivyojifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine, kwa mfano ya *hospitality* ni zaidi hata ya kujifunza darasani, lakini pale ni lazima mtu uweze ku-*gain competencies* ambazo zitaweza kukuwezesha kupambana kwenye soko la ajira; lakini haitafikia wakati tukaweza kumlazimisha mfanyabiashara kumwajiri mtu; isipokuwa tutajenga mazingira ya kuwawezesha Watanzania wawe washindani wazuri zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri; kwa vile utalii ni moja kati ya tegemeo kubwa la uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo Mabalozi hasa walioko nchi mbalimbali za *Latin America* na

*America* kuwa na uwezo wa kuweza kufanya ushawishi na kuweza kuunganisha Mashirika ya Kitalii yaliyoko katika nchi hasa za Ujerumani na Ufaransa kuweza kuja katika nchi zetu hizi na kuwa na mfano wa nchi ambazo wameweza kufanikiwa sana tukilinganisha nchi za Mauritius na nchi nyinginezo za Mashariki ya mbali ambazo zimefanikiwa sana katika suala hili la utalii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri alisimama. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kuniona, lakini napenda nianze kwa kweli kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sera ya Serikali ya *economic diplomacy,* hii ni moja ya nguzo ya kujenga mapato ya Serikali kwa kuzitumia Balozi zetu kutusaidia katika kutangaza utalii katika maeneo yao na tayari tumeanza kuandaa vitini ambavyo tutawapelekea Mabalozi ili hata mgeni akiingia kwenye Ubalozi wetu, ajue tayari ni vitu gani viko Tanzania. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane katika jambo hili ili kuweza kufanikisha sera hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Nitaleta kwenu matangazo; yako mengi kidogo. Nitaanza na matangazo ya Wageni.

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni jukwaa la Spika; na huyu ni mgeni wa Naibu Spika kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, yaani *UNDP* ambaye ni ndugu Hawa Dabo. Karibu sana. Huyu ni Mkurugenzi Mkazi wa *UNDP*-Tanzania. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kundi la kwanza ni Wageni 42 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Wanachuo wa Vyuo mbalimbali vilivyopo Dodoma wanaotoka Jimbo la Kyela. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni 41 wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Posi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu kutoka Baraza la Watoto Wenye Ulemavu Tanzania, wakiongozwa na Mchungaji Elias Shija ambaye ni Katibu Mkuu wa Kanisa la *FPCT.* Karibuni sana. Pia wameongozana na Ndugu Yohana

Dominic ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Watoto wenye Ulemavu Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni tisa wa Mheshimiwa William Ole-Nasha ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao ni Madiwani na Viongozi wengine kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Ndugu Mathew Siloma ambaye ni Mwenyekiti wa Wilaya, Halmashauri ya Ngorongoro. Karibuni sana. Wameongozana pia na Makamu Mwenyekiti wa Wilaya, Halmashauri ya Ngorongoro, Ndugu Kajurusi Dugo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni 30 wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ambao ni Wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Frank na Mchungaji Tarimo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni watatu wa Mheshimiwa Oliver Semguruka ambao ni Ndugu Edina Semguruka ambaye ni dada yake. Tunaye pia Ndugu Vanessa Kosamu ambaye ni mtoto wake na Ndugu Amini Idrisa Elias ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa *UVCCM* kutoka Kagera. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni wanne wa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ambao ni Wakulima kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ndugu Elias Matai. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ambao ni Wajumbe wa Umoja wa Wabanguaji Korosho Tanzania kutoka Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Ndugu Tumpale Magehema ambaye ni Mwenyekiti wa umoja huo na pia Ndugu Sophia Mtama ambaye ni Mweka Hazina. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 70 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi *Southern Highlands* iliyopo Mafinga, Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yako matangazo mengine. Tangazo la kwanza ni Kikao cha Kamati ya Katiba na Sheria leo tarehe 7 Juni, 2016, Mwenyekiti anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba na Sheria mkutane katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana. Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba mhudhurie uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, (2016/2017 - 2020/2021) utakaofanyika leo tarehe 7 Juni, 2016 saa 5.00 asubuhi mara baada ya kuahirisha Bunge katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma.

Vile vile tangazo hili limeambatana na tangazo lingine kwamba usafiri kutoka hapa Bungeni kuelekea Chuo cha Mipango utakuwepo hapo nje. Kwa hiyo, tukitoka tu tunaingia kwenye basi tunapelekwa kwenye uzinduzi wa huo Mpango wa Pili na Mgeni Rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, mnaombwa kufika bila kukosa. Hivyo tukitoka tu hapa tutakuta *bus* hapo nje.

Lipo tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta, anawatangazia Wabunge wote waliopata barua za kikao cha jana baada ya kuahirishwa Bunge kwamba Kikao hicho sasa kitafanyika leo baada ya kuahirisha Bunge pale *Canteen*. Sasa sijajua, nadhani Mheshimiwa Margaret Sitta awasiliane na hao Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wanatakiwa kwenda Chuo cha Mipango, Dodoma; kwa hiyo, aangalie muda mzuri wa kukutana nao.

Tangazo lingine linatoka katika Idara ya Shughuli za Bunge na linawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote Wakristo kuhudhuria ibada katika Jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Sasa hii saa 7.00 mchana pia Kamati ya Katiba na Sheria inakutana huko. Kwa hiyo, nadhani watakubaliana namna nzuri ya matumizi ya hiyo nafasi.

Tangazo lingine, linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Katibu wa Wabunge wa CCM, anawatangazia wafuatao kwamba wakutane katika Ukumbi wa Waziri Mkuu ghorofa ya kwanza, Jengo la Utawala. Hajaandika muda hapa, lakini nadhani watakutana labda baada ya uzinduzi wa Mpango wa Pili ambao utafanyika Chuo cha Mipango, Dodoma. Nitayasoma majina haraka.

Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mboni Mhita, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa George Mkuchika, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mheshimiwa Jasmine Tisekwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega; mtakutana na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Ukumbi wa Waziri Mkuu mara baada ya uzinduzi wa Mpango wa Pili tutakapokuwa tumerudi.

Tangazo lingine, Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM anawatangazia Wabunge wote Wanawake wa CCM kuwa leo kutakuwa na kikao. Yeye anasema mara baada ya kuahirishwa kwa Kikao cha Bunge; sasa nadhani hata hii itakuwa ni baada ya uzinduzi wa Mpango. Kwa hiyo, tutakaporudishwa hapa na *bus*, Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa CCM, Katibu anataka tukutane wote ukumbi wa Pius Msekwa.

Kuna tangazo lingine linatoka Bunge *Sports Club* na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja anawatangazia kwamba *Bunge Sports Club* jana ilipata magoli matano dhidi ya magoli mawili ya Waandishi wa Habari. Kwa hiyo, tunaipongeza timu yetu ya mpira wa miguu. Hapa nimewekewa majina ya nyota wa mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, amewekewa jina hapa kwenye mabano ambalo sitalisoma kwa sababu nisingependa Bunge lishtakiwe kwa kutumia jina la mtu maarufu sana ambalo liko *patented* huenda.

Vile vile na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, naye ana jina lake la uwanjani ambalo tukikutana nje nitawaambia, hapa siwezi kulitangaza kwa kuogopa mashtaka. *(Kicheko/Makofi)*

Pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawakumbusha Wanamichezo wote kuwa kwa mujibu wa Katiba ya *Bunge Sports Club* michezo inayotambuliwa ni: moja, Mpira wa Miguu (*Football), Netball*, Mbio za masafa mbalimbali, *Round Tennis, Valley ball,* Mpira wa Kikapu *(Basketball)*, Mpira wa *Meza (Table Tennis),* Vishale, yaani *Dats*, Kuvuta Kamba na *Draft. (Makofi)*

Hivyo basi, kutokana na orodha ya michezo tajwa hapo juu, tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote watakaopenda kushiriki kwenye michezo hiyo ambayo haijaanza mazoezi, wajiorodheshe kupitia kwa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ambao ni wafuatao:

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Faida Bakari na Mheshimiwa Cosato Chumi ili vifaa viweze kuandaliwa na utaratibu mzuri wa mazoezi uweze kufanyika. Kwa taarifa tu, Waheshimiwa Wabunge, nimeambiwa Kocha wa kuvuta Kamba ni Mheshimiwa Gama. *(Makofi)*

Vile vile Waheshimiwa Wabunge wafuatao ni Watendaji kwa nafasi zifuatazo; yaani Benchi la Ufundi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, leo Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Kamati zake mbalimbali. Kocha Mkuu upande wa Mpira wa Miguu ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, Kocha Wasaidizi ni Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir na Ndugu Mark Tanda ambaye ni Mtumishi, Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Pia yupo Nahodha wa Timu ya Mpira wa Miguu, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na huyu anasaidiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda. Benchi la Ufundi, Kazi Maalum, linaongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Al-maarufu Profesa Maji Marefu akisaidiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Aeshi Hilal. *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Wajumbe wake wa Kamati ya Utendaji wakutane leo Ukumbi wa Msekwa, naye anasema mara baada ya kipindi cha maswali kwisha. Nadhani hata wao watakaporudi na *bus*, watakutana mara baada ya kurudi kutoka kwenye uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia, Mwongozo huwezi kuomba nikiwa nimesimama.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Ulikuwa unaahirisha ndiyo maana nimekuwahi kabla hujatoka. Mwongozo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*